SHULE YA UPILI YA GATITU

KIDATO CHA TATU

MWANZO WA MUHULA WA TATU 2016

KISWAHILI 102/2

JINA.....DARASA.....NAMBA.....

1)UFAHAMU

Sanaa ya maonyesho ya urembo na mitindo imezidi kukua na kutia for a sana nchini na Afrika kwa jumla katika siku za hivi karibuni. Sanaa hii imebadilika sana kadri ya mpito wa wakati.Kinyume na hapo awali ambapo mashindano ya urembo yalihusisha uzuri wa sura pekee,katika enzi ya leo ,wawaniaji mataji mbalimbali huhitajika kudhihirisha kuwa wana maarifa na hekima ambapo hulazimika hata kueleza jinsi taji fulani wanaweza kulitumia kusaidia jamii iwapo wataibuka washindi.

Vilevile, wanamitindo wamekubali mitindo yenye asili ya kiafrika na inayoendeleza tamaduni za Afrika,badala ya kuiga mitindo ya kimagharibi.Kwa sasa Kenya na Afrika kwa jumla inajivunia mwigizaji maarufu wa Tuzo ya Oscar, Bi Lupita Nyongto na mwanamitindo wa kutajika Bi Ajuma. Ufanisi huu haungeweza kufikiwa iwapo Afrika ingeendelea kupapia na kuiga mitindo ya kimagharibi.

Kwa sasa maonyesho mengi ya urembo na mitindo yanasheheni mitindo iiiayosawiri utamaduni wa kiafrika kama vile matumizi ya khanga,vikoi na leso katika utengenezaji wa mavazi mbalimbali. Siku hizi tamasha huandaliwa katika shule za upili, vyuo vikuu na vyuo vya kiufundi humu nchini kama mbinu ya kukuza vipaji vya wanafunzi.

Katika kongamano la Kimataifa la la kuadhimisha miaka 50 ya maendeleo ya Kiswahili nchini Kenya lililoandaliwa na chama cha Kiswahili cha Taifa, CHAKITA, katika chuo kikuu cha kikatoliki, CUEA, kulibainika kuwepo haja ya sanaa ya mashindano ya urembo na mitindo kusawiri sura kamili ya Kiafrika.

Tamasha za urembo na mitindo zinasheheni vipengele vingi vya fasihi simulizi. Kipera cha fasihi simulizi husheheni sifa mahsusi ambazo hujidhihirisha kupitia tanzu zake anuwai. Fasihi simulizi hubadilika kulingana na mpito wa wakati, maendeleo na mabadiliko ya jamii katika nyanja za kisiasa kijamii na kiuchumi. Katika ulimwengu wa sasa, kuna mambo anuwai yanayoshirikisha wanajamii na yanayosheheni vipengele vya fasihi simulizi. Tamasha za urembo ni miongoni mwa shughuli zinazowakilisha fasihi simulizi ya jadi pamoja na kusawiri hali halisi ya ulimwengu wa sasa.

Baadhi ya sifa katika sanaa ya maonyesho ya mitindo na urembo zinazosawiri sifa za fasihi simulizi ni kama utendaji,hadhira,wahusika na ubunifu. Wanamitindo mbalimbali hupita jukwaani kwa maiao na miondoko mbalimbali ili kuonyesha mitindo anuai kama ya mavazi,nywele na urembo. Utendaji ni miongoni mwa sifa muhimu za fasihi simulizi ambapo mtambaji hutumia utendaji iii kuteka hadhira yake na kuwasilisha ujumbe anaokusudia kwa hadhira lengwa.

Tamasha za urembo haziwezi zikafanikishwa bila ya hadhira ambayo ni kiungo muhimu katika mashindano haya.Hadhira hufanikisha tamasha hizi kupitia ada ya kiingilio , kufanya tamasha hizi kufana kwa kushangilia wanamitindo mbalimbali na kuhakiki mitindo na wahusika. Hadhira ni muhimu kwani huwezesha kuchagua washindi na hata kuboresha mitindo kutokana na maoni ya uhakiki wao kwa wasanii.Hii ni sawa na fasihi simulizi, ambapo hadhira ilikuwa na umuhimu mkubwa katika kuifanikisha.

Wahusika ndio wanaoonyesha mitindo mbalimbali ya mavazi au urembo.Kando na kwamba urembo wa wahusika hawa huwa ni kigezo muhimu cha kuamua ufanisi wao katika mashindano hayo,ukakamavu wao na ustadi wa miondoko huchangia pakubwa kuboresha tamasha hizi na kuzifanya kuwa za kufana.Bila shaka, fasihi simulizi haiwezi lukami1ika bila kuwepo kwa wahusika ambao ni kiungo muhimu katilca kipera hiki.

Sharti msanii abuni mitindo mipya na mahsusi iii kuwapiku washindani wake. Mitindo hii huweza kubuniwa kutoka kwa matawi, maua, karatasi na kadhalika almuradi ivutie na kuwasilisha ujumbe unaokusudiwa kwa hadhira lengwa. Iii kufanikisha hili, mwanamitindo hana budi kuwa na ubunifu wa kiwango chajuu. Aidha fasihi simulizi huhitaji ubunitui katika uwasilishaji wake. Kwa mfano, itahitaji ubunifu wa hail yajuu kusimulia kisa kimoja kwa kutumia mbinu tofauti iii kukifanya kana kwamba kinasimuliwa kwa mara ya kwanza kila wakati mtambaji anaposimulia.

Vileviie,jinsi fasihi simulizi inavyoweza kuhifadhiwa kwa sasa kupitia kanda za video na filamu, tamasha za mitindo zinazohusisha utendaji hai huweza kuhifadhiwa katika video na filamu ambapo hadhira inaweza kurejelea kutazama mashindano hayo. Maleba huhusishwa kupitia mitindo mbalimbaii ya mavazi na nywele. Fasthi siniulizi vilevile hufanya vivyo hivyo. Hata hivyo tofauti kuu inayojitokeza kati ya fasthi simulizi ya jadi na tamasha za mitindo na urembo ni kwamba,kinyume na fasthi simulizi ambayo ni mali ya jamii, mitindo ya mavazi au nywele ni mali ya mm binafsi au aliyebuni ambapo mwenyewe ana haki miliki kisheria.

Maswali

a)Ipe taarifa hii anwani mwafaka (al. 2)

.....

b)Toa tofauti kati ya uhakiki wa wanamitondo wa awali na wa sasa. (al. 2)

.....

.....

c)'Uafrika unatukuzwa katika maonyesho ya urembo na mitindo' Thibitisha. (al. 2)

.....

.....

d)Linganisha namna mbili kati ya fasihi simulizi na sanaa ya maonyesho ya urembo na mitindo .(al. 4)

.....

.....

.....

.....

.....

e)Taja wanaomiliki

(i) fasihi simulizi..... (al. 2)

.....

(ii) Sanaa ya maonyesho ya urembo na mitindo.....

.....

f)Eleza maana ya msamiati ufuatao jinsi ulivyotiumiwa katika taarifa . (al. 3)

(i) Kutia fora .....

(ii) Kuwapiku .....

(iii) Maleba .....

.....

2)**UFUPISHO**

Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali yanayofuata

Aina fulani za kansa huwapata zaidi wanaume. Kansa ya tezi-kibofu, ya koromeo nay a mapafu ni baadhi ya hizo. Kansa ya tezi- kibofu huwalenga zaidi ya wazee wa umri wa miaka sitini na zaidi. Je, umewahi kujiuliza sababu ya akina babu kwenda haja ndogo mara kwa mara? Hii ni dalili mojawapo ya kansa. Zingine ni ugumu wa kupitisha mkojo, ugumu wa kuanza na kutoa mkojo, damu kwenye mkojo, maumivu ya mgongo na kadhalika. Mwisho, tezi-kibofu huzidi kwa ukubwa na kufungia mkojo kwa kutoka

Kansa zinazowapata zaidi wanawake ni: ya nyumba ya uzazi na mziwa. Kansa ya maziwa inatisha mno. Wanawake wenye umri wa miaka thelathini na mitano na zaidi wamo hatarini kuliko wote. Dalili za awali ni uvimbe unaohisika kwa ndani za maziwa kutoa usaha. Kansa ya maziwa huenea upesi na kuviambuiza viungo vilivyo karibu kama vile mapafu, ini na kadhalika

Ugonjwa huu hautambuliki kwa urahsi mwanzoni, husababisha uchungu wowote. Inependekezwa kwamba ukaguzi wa mara kwa mara unaweza kusaidia kugundua kansa kabla haijakomaa na kusambaa kote mwilini. Dalili ya awali hupatikana katika kiungo husika.

Madaktari wanapendekeza mambo kadhaa. Kwanza ni ukaguzi wa kibinafsi kwenye viungo vilivyo na uwezekano mkubwa wa kuambukizwa. Kasha jambo lolote lisilo la kawaida kama uvimbe, ugumu wa kumeza na kadhalika, liwasilishwe mara moja kwa daktari. Daktari atafanya uchunguzi wake na kuamua ni lipi linalomfaa mhusika. Kadhalika, ushauri zaidi ni kuhusu aina ya vyakula na mitindo ya kisasa ya maisha. Vyakula vilivyojaa protini zipatikanazo katika nyama na mayai ni miongoni mwa vyakula hatari. Mafuta kutokana na mimea hupendekezwa. Uvutaji sigara, unywaji wa pombe na baadhi ya vipodozi vya kisasa vyenye zebaki zaweza kuzidisha uwezekano wa kupata kansa. Tukizingatia masharti haya, tutaziba ufa na kujiepusha kujenga ukuta.

Saratani n kama sikio la kufa lisiloweza kusikia dawa. Ikigunduliwa mapema, matibabu huanzishwa kwa kutumia dawa, tiba kemikali, tiba ya miale ambayo huzichoma kwa miale chembechembe. Zilizoambukizwa.

Ikizidi, lisilo budi hutendwa. Huwa hakuna tena budi kiungo kuondolewa kwa upasuai ili kuokoa sehemu zingine za mwili na maisha kwa jumla. Kwa wahenga hawakushauri kukata pua ili kuunga wajihi?

Maswali

(a) Fupisha aya tatu za mwanzo kwa maneno 60-65 (al. 8)

Matayarisho

.....

.....

.....

.....

.....

Jibu

.....

.....

.....

.....

.....

.....

(b) Kwa maneno yasiyozidi 50, eleza njia zinazoweza kutumiwa kuzuia na kutibu saratani. (al. 7)

Matayarisho

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

Jibu

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

MATUMIZI YA LUGHA

a)Geuza sentensi hii katika ukubwa wingi.

(al. 2)

Mtu huyu atanunua mbuzi na ng'ombe mwaka ujao.

b) Tambua shamirisho katika sentensi ifuatayo. (al. 3)

Muliro alitumia makasi kumkatia gauni Immaculate

.....

c) Bainisha chagizo katika sentensi ifuatayo. (al. 1)

Magaidi huandaa mikutano yao kisirisiri wasijulikane.

.....

d)Changanua sentensi ifuatayo kwa kutumia michoro ya matawi. (al. 4)

Rashid na Rehema walitunga mashairi mazuri sana.

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....

e) Andika vipasuo ghuna viwili. (al. 2)

.....

f) Tambua na uanishe vishazi katika sentensi hii.

Mbuzi walioibwa jana wamepatikana salama. (al. 2)

.....

.....

g) Tambulisha aina za virai katika sentensi hizi. (al. 2)

(i) Miti ilipandwa kando ya mto.

ii Xavi amechezewa vibaya sana.

.....

h)Ainisha viambishi katika neno hili:Alimlisha (al. 3)

.....

.....

.....

i) Eleza matumizi ya maneno yaliyopigiwa mstari katika sentensi. (al. 1)

Haraka yao iliwafanya watembee haraka ili wafike mapema

.....

ISIMU JAMII

Taja mambo yoyote matano yanayofanywa na serikali yetu kuimarisha lugha ya Kiswahili (alama 10)

.....

.....

.....

.....

.....

.....

.....